



KIBABII UNIVERSITY COLLEGE

UNIVERSITY EXAMINATIONS

**2014/2015 ACADEMIC YEAR
FIRST YEAR SECOND SEMESTER**

MAIN EXAMINATION

**FOR THE DEGREE OF MASTER OF EDUCATION IN
KISWAHILI**

COURSE CODE: LEK 803

COURSE TITLE: TEACHING LITERATURE IN KISWAHILI

DATE: **TIME:**

MAELEKEZO

Jibu maswali **matatu** pekee.

MUDA: Masaa Matatu (3)

KIBUCO observes **ZERO** tolerance to examinations cheating

Maswali

1. Huku ukirejelea malengo yoyote manne yanayopatikana katika silabasi, bainisha namna malengo hayo hutimizwa kupitia ufundishaji wa mada mahsusini za Fasihi ya Kiswahili. (alama 20)
 2. Jadili kipengele cha utoshelevu wa silabasi ya Kiswahili nchini Kenya, hususan katika upande wa Fasihi. (alama 20)
 3. Fafanua nafasi ya andalio la somo na makadirio endegezi kwa mwalimu wa fasihi ya Kiswahili. (alama 20)
 4. “Somo la Fasihi linaweza kutathminiwa vizuri zaidi kwa kutumia tathmini endegezi badala ya tathmini tamati.” Pambanua kauli hii kwa kutumia hoja zozote tano. (alama 20)
 5. “Mwalimu wa Fasihi Simulizi anastahili kutumia mbinu za kipekee katika kufundisha.” Eleza. (alama 20)



KIBABII UNIVERSITY COLLEGE

(A Constituent College of Masinde Muliro University of Science and Technology)

Tel: 020-2028660 / 0708-085934 / 0734-831729
P.O. Box 1699-50200
Bungoma
Kenya

E-mail: enquiries@kibabiuniversity.ac.ke
Website: <http://www.kibabiuniversity.ac.ke>

LEK 803: TEACHING LITERATURE IN KISWAHILI

Mhadhiri: Dkt. F. C. N. S. Wanjala

Simu: +254726335079

Barua Pepe: simiyu57@yahoo.com

Utangulizi wa Kozi

Kozi hii inanuia kumtayarisha mwalifunzi kufundisha Fasihi ya Kiswahili katika shule za upili na vyuo nchini Kenya. Ni kozi ambayo inadhamiria kutoa elimu, ujuzi na maarifa mapya, mabadiliko na changamoto katika ufundishaji wa Fasihi ya Kiswahili, hasa kwa kuoanisha na malengo yaliyomo katika mtaala wa elimu wa Kenya.

Malengo ya Kozi

Kozi hii inalenga kudadavua masuala haya:

- Muhtasari wa somo la Kiswahili (fasihi) na kuifasili kulingana na mazingira ya darasani.
- Azimio la kazi na andalio la somo.
- Ujuzi wa kubuni mbinu mbalimbali za kufundisha vipengele vyote vilivyomo katika muhtasari wa somo la Kiswahili (fasihi).
- Zana mbalimbali zihusozo mada anuwai katika ngazi mbalimbali za ufundishaji wa somo la Kiswahili (fasihi) shule za upili.
- Tathmini ya yaliyofundishwa.

Matokeo ya Ujifunzaji

Kufikia mwisho wa kozi hii, kila mwalifunzi aweze:

- Kuchambua muhtasari wa somo la Kiswahili (fasihi) na kuufasili kulingana na mazingira ya darasani.
- Kutayarisha azimio la kazi na andalio la somo.
- Kubuni mbinu anuwai (ufaraguzi wa mbinu) za kufundishia vipengele vyote vilivyomo katika muhtasari wa somo la Kiswahili (fasihi).
- Kubuni na kutayarisha zana anuwai zihusuzo mada mbalimbali katika ngazi zote za ufundishaji wa somo la Kiswahili (fasihi) kwa shule za upili.
- Kutathmini ufanisi wa vipengele vyote vilivyofundishwa.

Mawanda ya Kozi

Mada ya 1. Fasihi na muktadha wake katika ufundishaji wa Kiswahili

- Maana ya fasihi
- Sifa za fasihi
- Aina za fasihi
- Sifa za mwalimu wa fasihi ya Kiswahili

Mada ya 2: Ufundishaji wa fasihi nchini Kenya

- Malengo ya kufundisha fasihi
- Mbinu za kufundishia fasihi
- Changamoto za kufundisha lugha na fasihi kwa pamoja

Mada ya 3: Uchambuzi wa muhtasari wa somo la Kiswahili

- Chimbuko, malengo, maudhui, mbinu za kufundisha, vifaa/zana na tathmini.
- Utoshelevu
- Utelelezaji
- Uchambuzi wa malengo
- Uchambuzi wa mada
- Mpangilio wa mada
- Azimio la kazi
- Andalio la somo
- Utoaji wa somo
- Tathmini ya somo

Mada ya 4: Maandalizi ya mwalimu

- Jinsi ya kuandaa azimio la kazi
- Jinsi ya kutayarisha andalio la somo
- Jinsi ya kutayarisha zana za kufundishia na kujifunzia
- Jinsi ya kuandaa nukuu za mwalimu

- Jinsi ya kutayarisha makadirio endelevi
- Jinsi ya kutayarisha hifadhi ya kazi

Mada ya 5: Tathmini

- Fasili ya istilahi “tathmini”
- Dhima za tathmini
- Aina za tathmini (tathmini endelevu na tathmini tamati)
- Uchambuzi wa mitihani anuwai

Tathmini ya kozi

- | | |
|--|-------|
| <ul style="list-style-type: none"> • Kazi-mradi (utafiti na uwasilishaji) • Mtihani wa mwisho wa semesta | = 40% |
| | = 60% |

Mbinu za Ufundishaji

Mhadhiri ataeleza kwa ujumla vipingele vyote vyatia kozitia mbinu ya mhadhara. Kisha, wanafunzi watapewa mada mbalimbali ili wazifanyie utafiti wa kina na kuwasilisha matokeo darasani. Kwa hivyo, mbinu zitakazotumiwa kufundisha kozitii hii ni pamoja na miadhara, mawasilisho na mijadala.

MAREJELEO

- Brumfit, C. J. (1970). *Language and Literature Teaching*. Oxford: Pergamon Press.
- Mbunda, F. (1977). *Ufundishaji wa Kiswahili Sekondari*. FED University of Dar es Salaam.
- Musau, P. na Chacha, L. 82001). *Mbinu za Kufundishia Kiswahili kwa Walimu wa Shule za Msingi, Upili na Vyuo*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Njogu, K. na R. Chimerah. (2008). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundations.
- Nduguru, S. (1986). *Kanuni na Mbinu za Kufundisha*. Dar es Salaam: Mbogo International Graphic Arts.
- Syambo, B. na wengine. (1987). *Jinsi ya Kufundisha Kiswahili katika Shule za Msingi*. Nairobi: Heinemann Kenya.
- Tuntufye, N. D. (1972). *Jinsi ya Kufundisha Kiswahili*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House Ltd.
- Wanjala, S. F. na J. M. Kavoi. (2012). *Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundishia Kiswahili*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.
- Wizara ya Elimu na Sayansi. (2005). *Muhtasari wa Kiswahili kwa Shule za Upili*. Nairobi: Taasisi ya Elimu Kenya.